

Maelezo ya Ripoti ya 15 ya TEITI

Ripoti ya kumi na tano (15) ya TEITI inatoa taarifa na takwimu za kodi zilizolipwa na kampuni za madini, mafuta na gesi asilia pamoja na mapato yaliyopokelewa na taasisi za serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Aidha ripoti hii inalinganisha malipo na mapato hayo kwa lengo la kubaini kama fedha zimeingia katika mfumo wa Serikali. Maandalizi ya ripoti hii yalitanguliwa na zoezi la uchambuzi wa kampuni zote zinazofanya shughuli za utafutaji na uchimbaji wa rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia katika mwaka wa fedha 2022/2023. Lengo la uchambuzi huo ni kubaini kiwango cha kodi kilicholipwa kutoka katika kampuni za madini, mafuta na gesi asilia.

Kulingana na kiwango cha chini cha malipo kilichopendekezwa na Kamati ya TEITI cha Shilingi 2,000,000,000, kampuni 58 zilichaguliwa kuingia katika zoezi la ulinganishi (zikihusisha Taasisi 3 (SoEs) zinazomilikiwa na Serikali). Kampuni zote 58 zilitakiwa kuwasilisha tatwimu kwa ajili ya maandalizi ya ripoti ya TEITI. Hata hivyo, kampuni arobaini na saba (47) tu, sawa na 81.03%, ndizo zilizowasilisha taarifa na takwimu kwa ajili ya maandalizi ya ripoti na kampuni kumi na moja (11), sawa na asilimia 18.97, hazikuwasilisha taarifa na takwimu kutokana na sababu mbalimbali. Ripoti ya 15 ya TEITI pia inajumuisha taarifa na takwimu kuhusu Ajira; Ushiriki wa Wazawa katika Sekta ya Uziduaaji (Local Content); Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii (CSR); Mfumo wa Sera na Sheria; Mchango wa Sekta ya Uchimbaji katika Uchumi; Maendeleo ya Sekta za uchimbaji; na taarifa nyingine kuhusu Mazingira, Jamii na Utawala (ESG).